BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** kila sifa njema ni zake Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vyote vilivyomo, kwa kutujaalia uhai na afya njema ambayo imetuwezesha kukutana tena kwa dhamira ya kujadili Bajeti kuu ya Serikali na Taasisi zake katika Baraza hili Tukufu. Kwani hii ni rehma yake Muumba kwa kutupa pumzi na afya njema ambayo wenzetu wengine amewanyima fursa hii na wameshindwa kutimiza malengo yao.

**Mheshimiwa Spika,** pia, napenda kutumia fursa hii adhimu kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele yako, kwa lengo la kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusiana na ***Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa mwaka wa fedha 2023/2024*** kama Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka *2020* zinavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, niwapongeze na kuwashukuru kwa dhati viongozi wa Ofisi hii wakiongozwa na Waziri wao hodari na mchapakazi Mheshimiwa Masoud Ali Mohammed, Katibu Mkuu Ndugu Issa Mahfoudh Haji na Naibu Katibu Mkuu wake Ndugu Mikidadi Mbarouk Mzee, Wakuu

wa Mikoa pamoja Afisa Mdhamini Pemba na watendaji wote kwa mashirikiano yao makubwa waliyotuonesha katika Kamati yetu na kupelekea kutekeleza majukumu yetu ipasavyo. Vile vile, shukurani za pekee ziende kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makamanda, Maafisa na Wapiganaji wote wa Vikosi vya Idara Maalum za SMZ kwa mashirikiano yao waliyotupatia kwa kipindi chote cha utekelezaji wa shughuli za Kamati katika kusimamia utekelezaji wa Bajeti zao.

**Mheshimiwa Spika,** kwa umuhimu wake, naomba kutumia nafasi hii kuishukuru Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kutumia na kutekeleza vyema ushauri na maagizo ya Kamati pamoja na kusimamia kwa ukamilifu na mipango ya utekelezaji wa programu zilizoainishwa katika Bajeti ya mwaka *2022/2023*, jambo hili limewawezesha kujenga ari ya kuwasilisha mbele ya Kamati yetu, pamoja na Baraza lako Tukufu Makadirio mapya ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka wa fedha *2023/2024* ili yapate baraka za Wajumbe wako na kwa muktadha huo, tunaliomba Baraza lako liridhie na liipitishe Bajeti hii kwa maslahi ya wananchi na Serikali kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, naomba kutoa shukrani na pongezi za pekee kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi imara wa Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi katika uongozi wake na kuhakikisha maendeleo ya watu na ustawi wa jamii nchini umeimarika kwa kuwainua wazee na wastaafu ambao wamelitumikia kwa nguvu kubwa Taifa hili pamoja na kusimamia mipango yote ya kimkakati kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee, nachukua nafasi hii kuwashukuru kwa kazi kubwa waliyoifanya Wajumbe wa Kamati yangu wakati tulipoipitia bajeti hii, kwa kuonesha umahiri na mashirikiano yao makubwa katika kutekeleza majukumu ya Kamati hii.

Naomba sasa niwatambue Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Zaina Abdulla Salum | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Mohamed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| *7.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *8.* | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *9.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imetumia vyema nafasi yake katika kupitia, kuchambua na kujiridhisha na programu zote zilizokusudiwa kufanyiwa kazi kupitia Mafungu ya Bajeti ya Wizara hii kama ilivyoelezwa katika Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Mwaka *2020*.

**Mheshimiwa Spika,** ni imani ya Kamati hii kwamba kupatikana kwa fedha zilizokadiriwa kutumika katika Ofisi hii kutasaidia kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa malengo yaliyokusudiwa katika kipindi husika ikiwa ni pamoja na kukamilisha miradi mbali mbali ya kimaendeleo.

**PROGRAMU ZA MAKAO MAKUU (FUNGU D 01)**

***Mheshimiwa Spika,*** kupitia programu kuu ya **PD0101** ya **Uratibu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;** Kamati inashauri mamlaka husika wakati wa kupanga makadirio ya mapato na matumizi ya Taasisi zenye kukusanya mapato pia, tuzingatie vyanzo vya mapato vya Taasisi husika na uwepo uwiano kati ya Taasisi moja na nyengine. Katika suala hili, Kamati kupitia mafungu ya Mikoa imegundua kwamba baadhi ya Mikoa ilipangiwa kukusanya kiwango kikubwa cha mapato bila kuangalia uwezo wa vyanzo vya mkoa husika.

***Mheshimiwa Spika,*** Katika programu ndogo ya **SD010102** ya **Uratibu wa Tawala za Mikoa** yenye lengo kuu la kuongeza ufanisi wa kiutendaji na upatikanaji wa huduma za jamii, Kamati yangu inapata mashaka kwamba lengo la programu hii halitofikiwa kutokana na changamoto za vifaa ambazo zinazikabili Halmashauri zetu, kwa mfano katika Mabaraza ya Miji ya Chake – Chake, Wete, Kaskazini A na Kaskazini B pamoja na Baraza la Mji Kati hawana magari ya maji taka. Ukosefu huu unazifanya taasisi hizi kushindwa kufikia malengo yake katika jukumu la usafi na hivyo kuonekana na nguvu ndogo ya kuweka miji safi na kuchangia miji yetu kutokuwa na haiba nzuri siku hadi siku.

***Mheshimiwa Spika,*** Kwa namna hiyo, Kamati inaiomba Serikali kupitia Bajeti hii kuanda mpango maalumu utakaoziwezesha Halmashauri zetu kupatiwa vifaa vya kisasa vyenye uwezo wa kufanyia kazi na kuleta malengo chanya. Kamati, pia inaziagiza Halmashauri na Mabaraza kuhakikisha miundombinu ya masoko ya UVIKO 19 imekamilika sambamba na kukamilika kwa ujenzi wa masoko hayo, kwa kuwa yapo baadhi ya masoko yameshakamilika lakini mpaka wakati huu hayajaunganishwa na huduma za umeme na maji na baadhi yake hayana hata sehemu za maegesho ya magari. Hata hivyo, Kamati inazishauri Serikali za Mikoa kusimamia changamoto hizo.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati yangu pia, inaitaka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kupitia programu ndogo ya **SD010101** ya **Uratibu wa Tawala za Mikoa** kuhakikisha wamesimamia vyema majukumu ya Halmashauri zaa ili kwenda sambamba na malengo ya Serikali. Kamati inawashauri wakuu wa Mikoa na Wilaya kuwapa uhuru wakurugenzi wao kufanya kazi kwa kutumia uwezo na taaluma zao ili kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Aidha, kamati inashauri kwamba wakati umefika kwa mafungu ya Halmashauri, ikiwemo Manispaa, Mabaraza na Halmashauri kusimamiwa na wakurugenzi wenyewe badala ya Makatibu Tawala kwa vile hoja zote za matumizi ya fedha hizo huwa wanahojiwa wakurugenzi hao badala ya Makatibu Tawala wa Mikoa.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati pia, haikuridhishwa na kasi ya ukusanyaji wa mapato kwa Halmashauri zetu kutokana na kiwango kidogo kilicho kusanywa na hivyo kushindwa kufikia malengo. Kamati imebaini kuwa upungufu huu unatokana na sababu ya msingi ya kukosekana kwa fedha za marejesho za maliasili kutoka Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kutopatikana kwa wakati na hivyo kupunguza kiwango cha fedha zilizokadiriwa kukusanywa na Halmashauri husika. Vile vile, uhaba wa vitendea kazi pia unachangia kupungua kwa mapato na kupelekea programu hii kushindwa kufikia malengo.

***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Programu ndogo ya **SD010404** ya **Kuratib Jumuiya zisizo za Kiserikali;** Kamati inazipongeza Jumuiya zote zinazofanya kazi hapa Zanzibar kwa lengo la kuisaidia Serikali kutatua matatizo ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Katika malengo ya kuanzishwa kwa Jumuiya hizo ni dhahiri kwamba zipo zinazofikia malengo na zipo zinazoshindwa kufikia malengo. Kamati pia, imebaini kuwepo kwa baadhi ya Jumuiya zisizofuata Katiba na Kanuni zao na hivyo kufanya kazi kwa kuvunja utaratibu uliowekwa kisheria.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati, inaishauri Wizara kuhakikisha imezifuatilia Jumuiya zote zinazovunja utaratibu na kufanya kazi zake bila kufuata Katiba zao. Kwa maana hiyo, tunashauri Jumuiya hizo kusimamishwa kufanyakazi Zanzibar na hatua nyengine za kisheria ziweze kuchukuliwa juu yao. Aidha, Kamati inaiomba Serikali na Jamii na ujumla kuthamini juhudi zinazofanywa na jumuiya hizi kwa lengo la kuhuisha maendeleo ya Zanzibar.

**PROGRAMU ZA IDARA MAALUM ZA SMZ (FUNGU D 02 – D 06):**

***Mheshimiwa Spika,*** Kwa upande wa programu za Idara Maalum za SMZ ambazo programu yake kuu ya Uratibu na Usimamizi wa Idara Maalum inatekelezwa kupitia **fungu D01** la Ofisi Kuu ili kuweka uwiano wa Idara zote za SMZ katika masuala ya kiutawala. Kamati imeridhishwa na kazi

nzuri za wapiganaji wetu wa vikosi vya SMZ kwa kushirikiana na vikosi vya SMT kwa kazi nzito wanazozifanya za kulinda, kusimamia na kudumisha usalama wa raia na mali zao pamoja na kuhakikisha tunu ya amani na utulivu tuliyonayo imedumu katika nchi yetu, tumuombe Mwenyezi Mungu azidi kutulinda na kuwapa uzalendo askari wetu wa kuitumikia vyema nchi yao.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati kupitia programu ndogo ya **SD0100201** ya **Usimamizi wa Utumishi na Uratibu,** Kamati inaishauri Tume ya Utumishi ya Idara Maalum kuhakikisha programu hii imekamilika na kufikiwa malengo yake kwa kuboresha mazingira ya kazi za askari wetu pamoja na kulinda maslahi yao katika nyanja zote ikiwemo matumizi ya vyeo, kulinda utaratibu wa kupandisha na kushusha vyeo, maposho ya likizo, maposho ya uhamisho na stahiki nyengine za kiaskari. Aidha, Kamati katika ziara zake za kawaida imebaini kuwepo kwa changamoto ya fedha za OC ambazo zitatumika katika uendeshaji wa ofisi, jambo ambalo linaathiri kwa kiasi kikubwa malipo ya stahiki za askari kama ilivyo kwa taratibu za kiutumishi.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati yetu inavishukuru na kuvipongeza vikosi vyote vya Idara Maalum za SMZ kwa kutekeleza vyema agizo la Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la kujiimarisha kiuchumi kwa kuanzisha miradi ya maendeleo ambayo italeta tija kwa vikosi hivi ili kuepuka utegemezi mkubwa wa ruzuku kutoka Serikalini. Aidha, Kamati inashauri vikosi hivi kuanzisha miradi kwa mujibu wa uwezo wao wa kifedha na kiutalamu, sambamba na upatikanaji wa masoko yakutosha kwa ile miradi yenye kuhitaji masoko. Aidha, Kamati inawaomba wananchi kuwa na uzalendo wa kununua na kutumia bidhaa zinazozalishwa na Idara Maalumu kwani zina ubora na zinaendana na mazingira yetu.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati inazidi kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa juhudi zake za kuviimarisha vikosi vya SMZ na kuimarisha maslahi ya wapiganaji wote wa Idara maalumu.

Aidha pongezi za pekee ziende kwa Wakuu wa Vikosi vyote vya SMZ kwa juhudi zao za kusimamia vyema majukumu waliyopewa pamoja na kuibua miradi mbalimbali ya kimaendeleo katika idara zao.

***Mheshimiwa Spika,*** katika mipango ya bajeti ya mwaka 2023/2024 kupitia Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo chenye **Fungu D04;** Kamati imeridhishwa na juhudi zao za kuibua miradi mipya na ya kimkakati katika kikosi. Kamati inaamini kwamba kutekelezwa kwa miradi hii kutasaidia KMKM kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kwa kiwango ambacho kimekadiriwa katika bajeti hii.

***Mheshimiwa Spika,*** pongezi pekee ziende kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kusimamia na kufuatilia vijana wanaojitolea JKU kwa ajili ya kujenga taifa. Hivyo, kupitia **Fungu D02 JKU;** Kamati inaishauri Serikali kuimarisha miundombinu ya mabweni na wakufunzi ili kuzidisha uwezo wa kuchukua vijana wengi kutoka na hamasa ambayo imepatikana katika miaka hii ya karibuni pamoja na kuimarika kwa maslahi ya vijana katika shughuli zao za kila siku.

***Mheshimiwa Spika,*** aidha, Kamati yangu haikufurahishwa na kitendo cha vijana wa kujitolea kulipwa fedha kwa njia ya hesabu za benki kwani kufanya hivyo, kutawafanya vijana hawa kuondoka makambini na kukimbilia mjini kwa ajili ya kufuata fedha za posho lakini pia kutakua na uwezekano mkubwa wa kulipwa vijana ambao wameshaondoka kwa njia mbali mbali kabla ya kumaliza mafunzo yao.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati pia, inaridhishwa na kazi za Wakala wa Ulinzi wa JKU ambao hutumika kama chanzo kikuu cha mapato katika kikosi hiki kuendelea kuimarisha huduma za ulinzi kwa taasisi wanazozifanyia kazi ili kuzidisha ulinzi na usalama kwa raia na mali zao. Aidha, Kamati inaendelea kusisitiza Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maaalum za SMZ kufuatilia kwa ukaribu zaidi madeni yote ya Wakala wa Ulinzi na kuhakikisha yanalipwa kwa mujibu wa taratibu. Hata hivyo, Kamati

inazishauri taasisi zinazodaiwa na wakala wa ulinzi kuhakikisha wamelipa madeni yao ndani ya kupindi hiki cha mwisho wa Bajaeti ya 2023/24 au Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuingilia kati madeni haya na kutafuta njia sahihi ya kulipatia ufumbuzi. Aidha, kamati inawapongeza Makamanda wa Jeshi la Kujenga Uchumi kwa kuimarisha skuli yao ya sekondari iliyopo Mtoni. Ni matarajio ya Kamati kwamba juhudi zaidi za kuimarisha Skuli hiyo ikiwemo vitendea kazi na kuajiri walimu wapya zitachukuliwa.

***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa **Fungu D03 -** Chuo cha Mafunzo Zanzibar, Kamati yangu pia, inawashukuru na kuwapongeza kwa kazi nzuri wanazozifanya chini ya Kamishna Mkuu kwa kuwalea, kuwatunza na kuwalinda vijana wetu walioko Chuo cha Mafunzo kwa Unguja na Pemba na kuhakikisha wanapotoka wamekua na tabia njema katika jamii.

***Mheshimiwa Spika,*** Aidha, Kamati imebaini kuwepo kwa mahabusu wengi katika Magereza yetu na wanaoongezeka siku hadi siku kutokana na vitendo vya uhalifu vinavyofanyika katika jamii. Kamati inaishauri Serikali kutenga fungu maalumu la bajeti kwa ajili ya mahabusu na wanafunzi ili kusiwe na fungu moja kati ya wao na askari wetu. Kufanya hivyo, kutasaidia Chuo Cha Mafunzo kutumia fedha zao kwa ajili ya shughuli za uendeshaji na maendeleo.

***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekelza vizuri majukumu ya Chuo Cha Mafunzo kutokana na wakati huu wa mabadiliko makubwa ya sayansi na teknolojia, Kamati imebaini kuwa Sheria Nambari *1* ya mwaka *1980* ina mapungufu ambapo kwa sasa haiendani na mahitaji halisi ya utelekezaji wa kikosi hicho licha ya juhudi kubwa kufanyika hapo nyuma za kuifanyia marekebisho lakini bado lengo halikufikiwa. Kamati inashauri Chuo cha Mafunzo kwa kushirikiana na Afisi ya Mwanasheria Mkuu kuifanyia mapitio sheria hii ili kurekebishwa na kwenda na wakati.

***Mheshimiwa Spika,*** katika **Fungu D05 –** Kikosi cha Zimamoto na Uokozi; Kamati inashauri Serikali kufanya tathmini ya hali za vituo vyote vya KZU

kwa Unguja na Pemba ili kufahamu uwezo wa vituo hivyo katika ubora miundombinu inayotumika. Aidha, itakuwa vyema kama Serikali itaanzisha mpango wa kuvifanyia matengenezo ili viweze kuwa na hadhi inayolingana na kazi husika licha ya kuwepo mpango wa kuvifanyia maboresho vituo hivyo ambapo umeshaanza kwa upande wa Kaskazini Unguja kupitia kituo cha Mahonda. Kamati pia, inashauri kuboreshwa kwa mazingira ya utendaji kazi katika kikosi hiki ikiwa ni pamoja na kulindwa maslahi ya watumishi wake.

***Mheshimiwa Spika,*** vile vile, Kamati inasisitiza umuhimu wa kuimarisha huduma za Zimamoto na Uokozi katika Kiwanja cha Ndege cha Zanzibar kwa kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa watendaji na wahudumu ambao ni wasaidizi wakubwa wakati wa kutokea ajali za moto, pia Serikali isimamie kufanyika mapitio ya Sheria nambari *7* ya mwaka *1999* ya Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar kwa lengo la kuimarisha uwezo wa Taifa wa kukabiliana na dharura kwa kutoa huduma kwa wakati na ufanisi.

***Mheshimiwa Spika,*** katika kujenga mazingira bora ya kazi na kuimarisha ari ya askari wa Kikosi cha Valantia Zanzibar kupitia **Fungu D06;** Kamati yangu imeridhishwa na juhudi za kuimarisha kikosi kwa kujenga mahanga mapya na nyumba za maafisa kwa kambi mbali mbali za Unguja na Pemba, kikosi pia kinaendelea kuimarisha maendeleo yake kwa kubuni miradi ya maendeleo ambayo itasaidia kukwamua changamoto zao. Aidha, Kamati imebaini kwamba barabara nyingi zinazoingia katika Kambi za KVZ ni mbovu sana na hazilingani na maboresha yanayofanywa katika kambi zao. Kamati inashauri kupitia mpango wa ujenzi wa barabara za ndani ambao unaendelea kwa kasi kubwa kuingizwa pia barabara za vikosi ambazo kwa asilimia kubwa wanatumia pia na wanchi waliokaribu na kambi hizo.

***Mheshimiwa Spika,*** Sambamba na hayo, Kamati pia inashauri Wizara kusimamia marekebisho ya Sheria ya Kikosi cha Valantia kukamilika kwa wakati kwani imeshafikia hatua nzuri na inahitaji maboresho machache ili

nao wapate kufanya kazi za kibiashara ikiwemo ulinzi na uzalishaji. Kamati inapongeza Kamandi yote ya KVZ kwa Kutekeleza vyema majukumu yao.

**WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII (FUNGU D 12):**

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati inaipongeza Ofisi ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii kwa kuweka programu kuu ya **Kusajili vizazi, vifo na Kadi za Utambulisho;** kuwa na malengo ya kuimarisha huduma za usajili kwa ufanisi na kutoa vyeti pamoja na vitambulisho kwa wakati. Kamati inaiomba Taasisi hii kuzidisha kasi ya utoaji wa vyeti kwa njia ya kielektroniki kwa lengo la kuwapunguzia wananchi usumbufu na pia kutarajia kuimarika kwa taarifa za kijamii. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kufanya mpango wa ujenzi wa Ofisi mpya ya Matukio ya Kijamii katika Wilaya ya Wete Pemba kutokana na changamoto kubwa ya ofisi ambayo inawakabili tofauti na Wilaya nyengine ambazo zinaofisi nzuri na mazingira bora ya utendaji. Kamati baada ya tafakari ya kina inaishauri Serikali kuwapataia retention ya 25% ya fedha wanazokusanya ili kukabiliana na changamoto zinazowakabili.

**HITIMISHO:**

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati yangu inaomba kutoa wito kwa jamii kuhakikisha wanajisajili upya kila inapobidi kufanya hivyo, kwani sheria imebainisha matukio mbali mbali ambayo yanapaswa kusajiliwa ili Serikali iweze kutekeleza vyema mipango yake.

***Mheshimiwa Spika,*** pia, naomba niwashukuru Makamanda wa Idara Maalum za SMZ, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya, Wakurugenzi, Madiwani, Masheha na watendaji wote wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa utendaji wao na uzalendo wao, na mashirikiano yao katika kutekeleza majukumu ya Kamati yetu katika kipindi chote cha maisha ya Kamati hii.

***Mheshimiwa Spika,*** kwa kumalizia Kamati imeona kwamba majukumu mengi ya taasisi za Serikali hayawezi kufanyika ipasavyo kutokana na kutoingiziwa fedha kwa wakati na kwa mujibu wa kilichopangwa katika bajeti zao. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuingiza fedha kwa wakati na kama zilivyopangwa ili ufanisi wa kiutendaji uweze kupatikana kwa maendeleo ya wananchi na nchi yetu kwa ujumla.

***Mheshimiwa Spika,*** mwisho kabisa, Kamati inawaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu wairidhie, waichangie na waipitishe Bajeti hii na hatimae waidhinishe makadirio ya fedha zilizopangwa kutumiwa kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

**Mheshimiwa Spika,** *Kwa Niaba ya Kamati yangu;*

**Naomba Kuunga Mkono Hoja.**

Ahsante,



……………………………………

(Machano Othman Said)

**Mwenyekiti,**

**Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,**

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

**ZANZIBAR**